



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojobu tafdhali taja:
Kumb. Na. NGOR/DC/A.1/12/VOL.1/97

Tarehe: 29.05.2024

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea kibali cha ajira Mbadala chenye **Kumb. Na FA.228/613/01/B/071** cha tarehe **02 Aprili, 2024**

Kufuatia Kibali hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kutuma maombi ya kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kuanzia tarehe **29 Mei 2024** hadi **11 Juni, 2024** kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal)

1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III NAFASI (1)

1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Kujiriwa mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo Cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI

- I. Afisa Masuuli na mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji;
- II. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji;
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji;
- IV. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji;
- V. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- VI. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- VII. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya klitaalam katika kijiji;
- VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji;
- IX. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji;

- X. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- XI. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji; na
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa Kata.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya mshaharaa **TGS B**, sawa na Tshs. **450,000/=** kwa mwezi.

1.4 MAELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI


- a) Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu/Taaluma, cheti cha kuzaliwa, CV.
- b) Waombaji wa nafasi hii wanalazimika kuwa na namba ya Utambulisho wa Uraia National Identification Number kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- c) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika.
- d) "Testimonials", "Provisional results", "Statement of Results" na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (Form iv na Form VI result slips) havitapokolewa.
- e) Waombaji wenge ulemavu wanahamasishwa kuomba nafasi hii na wanashauriwa kuainisha aina ya ulemavu walionao

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **11 Juni, 2024**

Maombi yote yatumwe Kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (*Recruitment Portal*) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz> (Anuani inapatikana kwenye tovuti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa **Recruitment Portal**).

Maombi ambayo yatawasilishwa nje ya utaratibu uliotajwa hapa hayatashughulikiwa.

Tangazo hili limetolewa na


Murtallah S. Mbillu,
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

